



TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA
Kitalu Na. 339, Mtaa wa Nyerere - Kilimani
S.L.P 4019, DODOMA
Simu: +255 734 047 775; 734 119 978
Barua Pepe: info@chragg.go.tz
Tovuti: www.chragg.go.tz

Septemba 09, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Tamko la THBUB kulaani Mauaji ya Bw. Ally Mohammed Kibao – Mjumbe wa Sekretarieti ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA)

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imepokea kwa masikitiko makubwa kifo cha Bw. Ally Mohammed Kibao, Mjumbe wa Sekretarieti ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) aliyeuawa na watu wasiojulikana na kutupwa eneo la Ununio Jijini Dar es salaam. Taarifa kutoka vyanzo mbalimbali vya habari zinasema kuwa tarehe 6 Septemba, 2024 majira ya saa 12 jioni Bw. Ally Mohammed Kibao, akiwa safarini katika basi la Tashrif lenye Namba za usajiri T 343 EES lililokuwa linatoka Dar es salaam kuelekea Jijini Tanga alichukuliwa na kushushwa na watu wasiojulikana wakiwa na silaha pamoja na pingu baada ya magari mawili aina ya Toyota Landcruiser Hardtop yasiyokuwa na namba za usajili

kuzuia basi hilo katika eneo la Kibo Complex – Tegeta ambapo watu wawili waliingia ndani ya gari na kumfunga pingu Bw. Ally Mohamed Kibao kisha kumshusha na kuondoka naye kwenda kusikojulikana.

Aidha, tarehe 7 Septemba, 2024 zilipatikana taarifa kuhusu kupatikana kwa mwili wa Bw. Ally Kibao katika eneo la Ununio Jijini Dar es salaam. Taarifa hizo zilithibitishwa na Katibu Mkuu wa CHADEMA Ndugu. John Mnyika alipokuwa akiongea na Vyombo vya Habari Jijini Dar es salaam kuwa mwili wa Bw. Ally Kibao umekutwa ukiwa na majeraha makubwa usoni.

Tukio hili limetokea wakati THBUB inaendelea na kazi ya kufuatilia matukio kama haya yanayoendelea nchini. Matukio kama haya yanarudisha nyuma jitihada za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuimarisha ulinzi, amani na usalama wa raia na mali zao nchini.

THBUB inatamka kuwa tukio hilo la utekaji na mauaji ni:

- i) Ukiukwaji wa haki ya kuishi kama ilivyotamkwa katika Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na hivyo inalaani vikali vitendo hivyo;
- ii) Ukatili dhidi ya binadamu ambao ni kinyume na Ibara ya 13(6)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977;

- iii) Ukiukwaji wa haki ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru kama ilivyotamkwa katika Ibara ya 15(1)(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;
- iv) Ukiukwaji wa haki ya kwenda kokote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuishi katika sehemu yoyote kama mtu huru kama ilivyotamkwa katika Ibara ya 17(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;
- v) Ukiukwaji wa msingi wa utawala bora hususan utawala wa Sheria.

THBUB inatambua maelekezo ya Mhe. Dkt. Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa vyombo vya uchunguzi kufuatilia na kuwasilisha taarifa za kina kuhusu tukio hilo la kikatili na mengine ya namna hii yanayoendelea kutokea nchini, THBUB inaendelea na kazi ya uchunguzi kwa matukio mengine ya namna hii, ikiwa na pamoja na hili na itatoa taarifa yake kwa umma.


Aidha, THBUB inatoa wito kwa wananchi kutoa ushirikiano kwa THBUB na vyombo vingine vya dola vinavyochunguza tukio hili.

Mwisho, THBUB inatoa pole kwa viongozi na wanachama wa CHADEMA, familia, ndugu, jamaa na marafiki wa Bw. Ally Kibao kwa msiba mzito wa kumpoteza mpendwa wao. THBUB inawaasa wananchi wote kuwa watulivu na wenye subira hasa

katika kipindi hiki ambacho vyombo vya dola vinaendelea na uchunguzi wa tukio hilo.

Jukumu la ulinzi na utetezi wa haki za binadamu ni letu sote!

Imetolewa na:



Mathew P.M. Mwaimu (Jaji Mstaafu)
Mwenyekiti

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Septemba 09, 2024